Una Moyo Wa Aina Gani?

na

Ellis P. Forsman

Una Moyo Wa Aina Gani?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Una Moyo Wa Aina Gani?

Matendo Ya Mitume 2:

Je umewahi kufikiria kuhusu idadi ya watu waliotii injili siku ya Pentekoste? (Mdo. 2); vile vile, je umewahi kushangaa ni kwa nini watu wengi hawatii injili?

Hii ni kweli, hata ivyo Yesu alionja mauti kwa ajili ya watu wote.

Ebr. 2:9, "*Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.*"

Yesu alikufa kwa wasio na Mungu.

Rum. 5:6, "*Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu.*"

Na Mungu hapendi ye yote apotee.

2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*"

Wengi "wanao tembelea" upande mwingine – wakikataa wito wa Mungu na neema.

2 Thes. 2:14, "*Aliyowaitia ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Biblia inafundisha kwamba ni wachache watakao okolewa.

Njia imesonga na ni nyembamba.

- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia , Mimi ndimi njia na kweli na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi.*"
- Mt. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"

Ulimwengu wote umelala katika giza.

- 1 Yoh. 5:19, "*Twajua ya kuwa sisi tu wa Mungu; na dunia yote pia hukaa katika yule mwovu.*"
- Mt. 22:14, "*Kwa maana waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache.*"
- Mt. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.*"

Yesu anatufundisha wazi ni kwa nini wachache tu wataokolewa:

Mfano wa mpanzi. Luka 8:5-15, "*Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake, ; naye alipokuwa akizipanda, zingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila. Nyingine zikaanguka penye mwamba; zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba. Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga. Nyingine zilianguka penye udongo mzuri; zikamea zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, Mwenye masikio ya kusikia na asikie. Wanafunzi wake wakamwuliza, maana yake nini mfano huo? Akasema ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme wa Mungu; bali wengine kwa mifano, ili wakiona wasione, na wakisikia, wasielewe. Na huo mfano maana yake ni hii; Mbegu ni neno la Mungu. Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja Ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka. Na wale penye mwamba, ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga. Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote. Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia.*"

Yesu alisema wachache watafaulu.

Kwa nini? Sio kwa sababu Mungu hawapendi.

Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Tatizo linaegemea katika roho za wanadamu.

Katika somo hili, tunataka kujifunza aina nne za roho, ambayo kimsingiinawakilisha nafasi ya wote wanaosikia neno la Mungu, na tuone ni kwa nini wachache pekee wataweza.

Moyo ambao Shetani anatunza:

Zingatia mistari miwili hii:

- Luka 8:5, "*Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake; naye alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila.*"
- Luka 8:12, "*Wale wa karibu na njia ndio wale wasikiao, kisha huja ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka.*"

Tunajifunza hapa kwamba shetani yupo kila wakati Neno linapopandwa. Hataki uwezo wa Mungu iwe na njia yake. Shetani hakosi katika mkutano, mikusanyiko ya kanisa, n.k.

Kuna njia nyingi ambazo shetani hutumia kwa kuiba Neno katika mioyo za watu.

- Kupitia uongo na kudanganya (Adamu na Hawa). Shetani ni baba wa uongo wote.
- Kwa kukufanya uchelewe kutii kama Agripa alivyofanya. Anakutaka uamini kuwa bado una muda mwingi.
- Anakuchanganya kwa mafundisho ya uongo kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu.
- Anajaribu kukushawishi kwamba maisha ya dhambi ni bora.
- Anakutaka uamini kwamba uko sahihi.

Shetani yuko katika swala la kuiba neno. Usimruhusu aibe Neno kutoka katika moyo wako.

Moyo ambao majaribu huipata:

Zingatia hivi vifungu viwili:

- Luka 8:6, "*Nyingine zilianguka penye mwamba; zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba.*"
- Luka 8:13, "*Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga.*"

Hii inatupatia picha kwamba, kwa furaha kubwa, baadhi wanatii neno. Neno linaingia katika moyo na kukaa kwa muda mfupi.

Shetani haachi. Anatega mtego, au aibu.

1 Pet. 5:8, "*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze.*"

Majaribu yanayosababisha kuanguka yametapakaa kwa kila mtu. Mkristo <u>anaweza</u> kuanguka.

- 2 Pet. 2:20, "*Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu.*"
- Gal. 5:4, "*Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki <u>kwa sheria</u>; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema.*" (Sheria ya Musa).

Kifungu kinafunua kwamba hawa wanaanguka kwa sababu hawana mizizi.

Lazima tuwe na shina katika upendo na Neno la Mungu.

- Efe. 3:17-18, "*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana na urefu, na kimo, na kina,*"
- Kol. 2:6-7, "*Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kuoa shukrani.*"
- Yakobo 1:14-15, "*Lakini kila mmoja hujaribiwa na tama zake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Alafu ile tama ikiisha*

kuchukua mamba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti."

Wakristo lazima wakimbie kutoka katika muonekano wo wote wa uovu.

1 Thes. 5:22, "*Jitengeni na ubaya wa kila namna.*"

Hapaswi kwenda katika tabia yake ya zamani ya maisha. Lazima akumbuke kwamba yeye ni "mtoto."

1 Pet. 2:1-2, "*Basi wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote. Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu;*"

Moyo ulioshindwa na kujali, starehe, na utajiri

Zingatia mistari hii miwili:

- Luka 8:7, "*Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga.*"
- Luka 8:14, "*Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote.*"

Hawa, vile vile, hupokea Neno. Wanatii. Alafu wanakua. Baada ya muda kitambo kitu fulani kinatokea.

Wanatibuliwa. Wana "dumaa" au "kusukumwa," sawa na mtu adumazwe katika hali ya kimwili. Hawa wamejikwaa au wamechukuliwa kiroho.

Kuna vitu vingi vinavyoangamiza maisha yao ya kiroho:

Kujali. Hii inaweza kuwa kujali kuhusu kitu cho chote; kama vile, chakula, mavazi, kazi, afya, n.k. Lazima tufanye yale tunayoyaweza, alafu zingine tumrudishie Mungu.)

Mt. 11:28-30, "*Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo mizito, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.*"

Utajiri. (Kupenda au kutamani fedha, au ni nini itakacho nunua.)

Yak. 5:1-7, "*Haya basi enyi matajiri! Lieni mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia. Mali zenu zimeoza, na mavazi yenu*

yameliwa na nondo. Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho. Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi. Mmefanya anasa katika dunia, na kujifurahisha kwa tama; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo. Mmehukumu wenye haki mkamwua; wala hashindani nanyi. Kwa hiyo ndugu, vumilieni, hata kuja kwake Bwana. Tazama, mkulima hungoja mazao ya nchi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya mwisho."

Starehe. (Hali ya tamaa. Kuweka vitu vya dunia mbele za Mungu. Hatupaswi kuipenda dunia.)

Yak. 4:1-7, "*Vita vyatoka wapi, na mapigano yaliyoko kati yenu yatoka wapi? Si humu, katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viungo vyenu? Mwatamani wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu. Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu. Au mwadhani ya kwamba maandiko yasema bure? Huyo Roho akaaye ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu? Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu. Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.*"

"Hawaleti matunda katika ukamilifu." Wanaanzisha vitu vingi, lakini hawazikamilishi.

Lazima tukamilishe kile tulichokianzisha.

Luka 9:62, "*Yesu akamwambia, mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu.*"

Lazima tukamilishe mbio.

2 Tim. 4:6-8, "*Kwa maana mimi sasa namminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mkuhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*"

Kujali, utajiri, na starehe za dunia hii vitakusababisha upoteze roho yako.

Roho inayoitengeneza

Zingatia vifungu hivi viwili:

- Luka 8:8, "*Nyingine zilianguka penye udongo mzuri; zikamea, zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, Mwenye masikio ya kusikilia, na asikie.*"
- Luka 8:15, "*Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia.*"

Moyo kama huu unatazamwa kama "*Udongo mzuri.*" Ni moyo ulioandaliwa.

Roho bora zinazoweza kufika mbinguni.

Ni moyo mkarimu.

Moyo mkarimu utatafuta ukweli, na kuukubali.

- Yoh. 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"
- Yoh. 17:17, "*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*"
- Mt. 5:6, "*Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.*"

Moyo mkarimu unabadilika.

- Mdo. 2:37, "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje ndugu zetu?*
- Mdo. 8:27-40, "*Naye akaondoka akaenda mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena je yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake*

umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema nakuomba, nabii huyu; asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, tazama, maji haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi, naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria."

Ni moyo mwema.

Safi na takatifu. Mt. 5:8, "*Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu.*"

Ni moyo wa msamaha. Mt. 6:14-15, "*Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa Mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu wa mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.*"

Inasikia Neno. Inautayari wa kujitoa.

- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Mungu.*"
- Yako. 1:19-21, "*Hayo mnajua ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu.*"

Ni mtendaji wa Neno.

Yak. 1:22, "*Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.*"

Huzaa matunda.

Gal. 5:22-25, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.*"

Mzabibu na matawi.

Yoh. 15:1-14, "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu ninyi ni matawi akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya lo lote. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa mje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake. Hayo nimewaambia ili furaha yangu iwe ndani yenu na furaha yenu itimizwe. Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu mkitenda niwaamuruyo.*"

Ni moyo mkarimu.

Unavumilia. 1 Kor. 15:58, "*Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.*"

Kama Ayubu aliyekuwa mzee. Yak. 5:11, "*Angalieni twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma.*"

Inadhania ya kuwa inachukua muda kukua, kung'aa, na kutoweka.

Hitimisho

Ndiyo, wachache wataweza.

Moyo ulio na kazi njema na nia inaweza ikaweza.

Je una moyo wa aina gani?

Lazima uwe mpole wewe binafisi na Mungu.